# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA PILI

**01 NOVEMBA, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA PILI – TAREHE 01 NOVEMBA, 2023

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA AFYA:

Maelezo ya Waziri wa Afya kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022.

### MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**7. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni Wanawake wangapi wamekuwa Wabunge wa Majimbo na Madiwani katika chaguzi tatu mfululizo zilizopita.

**8. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali itaridhia Mkataba wa C189 wa Wafanyakazi wa Majumbani.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**9. MHESHIMIWA CHARLES JOHN MWIJAGE (MULEBA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka *Fibre Speed Boat* mbili zilizofunikwa kama *ambulance* ili kusaidia Wananchi wa Visiwa 39 vya Muleba.

**10. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itagawa Kata za Matiri, Litumbandyosi, Linda, Mkumbi, Litembo, Nyoni, Maguu na Langiro Wilayani Mbinga.

**11. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha upatikanaji wa Vifaa kwa Maabara za Sayansi katika Shule za Mkoa wa Katavi.

**12. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA (NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali italeta Sheria ya kuruhusu Halmashauri kutumia Benki kama wakala wa ukopeshaji na ukusanyaji madeni.

## OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

**13. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua na kutangaza maeneo ya uwekezaji Mkoani Kigoma.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**14. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali haioni kigezo cha uzoefu katika kuomba kazi ni ubaguzi dhidi ya Vijana waliohitimu Vyuo wanaolenga kuingia katika soko la ajira.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**15. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuelekeza Taasisi kununua Vyuma na Vipuri katika Kiwanda cha Kilimanjaro *Mashine Tools.*

**WIZARA YA KILIMO:**

**16. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itazilipa fedha Kampuni za Usambazaji wa Mbolea na Viuatilifu Mtwara.

**17. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia Televisheni ya Taifa na Redio kutoa elimu ya kilimo salama na chenye tija.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**18. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali italipa fidia kwa Wananchi 438 waliofanyiwa uthamini kupisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kilwa - Masoko.

**19. MHESHIMIWA RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN (CHAKECHAKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga Gati la Kisasa la Abiria kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

**20. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhusisha Majeshi ya Ulinzi na Usalama katika kulinda miradi mikubwa ya kimkakati.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**21. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, kwa nini Sheria za Ardhi zinazokusudiwa kutumika kwenye Miji zinatumika maeneo ya Vijijini.

**WIZARA YA AFYA:**

**22. MHESHIMIWA ALEKSIA ASIA KAMGUNA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga uzio katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro.

**WIZARA YA FEDHA:**

**23. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kuna mpango gani wa kuweka Kituo cha Forodha Kakozi Momba ili kuunga mkono jitihada za kujenga Soko la Mazao la Kimataifa.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**24. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itatoa idhini kwa Makampuni binafsi kutoa elimu ya kujikinga na majanga ya moto kwa Wananchi na Taasisi nchini.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**25. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha VETA Wilayani Kakonko.

**WIZARA YA MAJI:**

**26. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO (BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatekeleza mradi wa maji wa Darakuta-Magugu-Mwada hadi Minjingu - Babati.

**27. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa kupeleka maji Kata sita za Izimbya, Kyaitoke, Mugajwale, Ruhunga, Katoro na Kaibanja kutoka Ziwa Ikimba utaanza.

**WIZARA YA MADINI:**

**28. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali imefanya utafiti kuhusu uwepo wa Madini Mkoani Mtwara.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**29. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini elimu ya uvuvi, mikopo na vifaa vya kisasa vitatolewa maeneo ya Manda, Ruhuhu, Iwela, Lupingu, Lifuma, Makonde, Kilondo na Lumbila.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote wa Mwaka 2022.

**DODOMA** — **N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**01 NOVEMBA, 2023** — **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA